TOLEO NO.74

# Khilafah

DHULQA'ADA 1447 HIJIRIA —MEI 2026 MILADIA ( Bei Tsh 4,000/= - Ksh 200/=)

NDIO SULUHISHO

## UBEPARI CHANZO CHA VURUGU DHIDI YA WAHAMIAJI AFRIKA YA KUSINI



Kwa mara nyengine tena Afrika ya Kusini imegubikwa na wimbi la vurugu za ubaguzi kwa baadhi ya raia wake kuvamia kuwadhuru kikatili wahamiaji kutoka nchi za Afrika. Wimbi hili linaloambatana na maandamano linapinga uwepo wa wahamiaji haramu kutoka nchi za Afrika ambapo waandamanaji wanadai kwamba serikali yao imekua dhaifu dhidi ya wahamiaji hao.

Vurugu hizo zimeshagharimu maisha ya raia kadhaa hususan wa Nigeria, huku Kamati ya Haki za binadamu ya Umoja wa Afrika ikilaani vikali matendo hayo na kuitaka serikali ya Afrika ya Kusini kujizatiti kuzuuiya hali hiyo.

Katika hotuba yake katika Maadhimisho ya Siku ya Uchaguzi Huru juzi tarehe 27 Aprili 2026, siku kama hiyo mwaka 1994 ulipofanyika uchaguzi wa kwanza huru na usiokuwa wa kibaguzi Afrika ya Kusini, raisi wa nchi hiyo Cyril Ramaphosa alitumia maadhimisho hayo kulaani matendo hayo dhidi ya wageni, akiwakumbusha watu wa Afrika ya Kusini kwamba nchi yao ina deni kwa mataifa mengine ya Afrika kwa kuwaunga mkono dhidi ya mapambano yao dhidi ya ubaguzi wa rangi

Suala la chuki dhidi ya wageni sio jambo la Afrika ya Kusini pekee. Bali limekita kila mahala chini ya mfumo huu wa kibepari, lipo katika madola ya Magharibi pamoja na Marekani, nchi zinazoitwa vigezo vyema vya demokrasia.

Itakumbukwa kwamba uvamizi unaotokamana na chuki dhidi ya wageni umekuwa ni jambo maarufu nchini Afrika ya Kusini kwa muda sasa.

Mnamo mwaka 1994 na 1995 vijana waliokuwa na silaha walivunja nyumba za wageni mjini Johannesburg, wakiwataka polisi kuwarejesha raia hao

**Inaendelea Uk. 3**

## UINGEREZA KUPITIA JUKWAA LA JUMUIYA YA MADOLA WAENDELEA KUHIFADHI USHAWISHI WAO TANZANIA KIJANJAJANJA



Mnamo tarehe 8 Aprili 2026, Mjumbe Maalum wa Jumuiya ya Madola, Dkt. Lazarus Chakwera, rais wa zamani wa Malawi, aliwasili Dar es Salaam kwa lengo la kuhamasisha kuasisiwa mazungumzo baina ya wadau mbalimbali ili kupunguza mvutano wa kisiasa na malalamiko yaliyojitokeza kufuatia uchaguzi mkuu wa tarehe 29 Oktoba 2025. Mjumbe huyo Maalum aliteuliwa tarehe 17 Novemba 2025 kama sehemu ya juhudi za Jumuiya ya Madola kushughulikia ghasia zilizohusiana na uchaguzi mkuu wa Tanzania wa mwaka 2025.

Baada ya Programu za Marekebisho ya Kimuundo (SAPs) za miaka ya 1980 zilizolazimishwa na mataifa ya kibepari kwa Tanzania na nchi nyingine zinazoendelea kupitia Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia, ambazo zililenga na kusukuma sera za

**Inaendelea Uk. 7**

### Yaliyomo :



- **Ibada ya Hijja inahitaji Khilafah ……………………..……………..…...2**
- **Nusra Inatafutwa Kutoka Kwa Nani?! ………...………...……………4**
- **Mkataba wa Hilf al-fudhoul utuongeze hima ya ulinganizi……...6**

# IBADA YA HIJJA INAHITAJI KHILAFAH

Tayari ni msimu wa maandalizi ya mwisho wa Hijja ya mwaka huu wa 1447 Hijria yamepamba moto. Ibada hii inahitaji usimamizi kabambe na thabiti kinyume na hali ilivyo sasa. Leo ibada hii imegubikwa na kila uzito na vikwazo kwa kuachiwa usafirishaji wa mahujaji kwa taasisi binafsi na kumalizikia baadhi ya taasisi hizo kuwatapeli mahujaji au kuwachelewesha nk.

Aidha, usumbufu mkubwa zaidi unatokana na dola kibaraka ya kifalme ya Saudia kwa kuweka shehena ya vikwazo na urasimu usiokua wa lazima kuanzia gharama za unyang'anyi na dhulma ya kile wanachodai ati 'viza ya Hijja', ubaguzi wa kuwafanya wasiokuwa raia wa Saudia kama wageni wa daraja la pili kwa kuwang'ang'aniza vitambulisho maalum vya kibaguzi. Bila ya kutaja ***matumizi mabaya*** ya jukwaa la Hijja kama njia ya kukuza fikra potofu kama 'dini mseto', 'ubaguzi wa kimaeneo',fikra za kidemokrasia na kuchawanya maelfu majasusi kuwachunguza mahujaji ili wasipate fursa ya mawasiliano na ndugu zao wa kiislamu wa sehemu nyengine.

Hayo na mengine mengi ni matokeo ya ibada hii kutokua na msimamizi rasmi muadilifu na kiongozi wa Umma wa Kiislamu. Katika sharia ya Kiislamu jukumu hilo ni la Kiongozi rasmi wa Kiislamu (Khalifah). Katika kitabu cha 'Taarikhu-ul Umamil – Islamiyah' mwandishi anaeleza bayana kwamba: ***'katika kazi kubwa za Khalifah ni kusimamia Hijja'.***



Kama alivyokua Mtume SAAW akisimamia mwenyewe ibada hii kama alivyofanya katika Hijja ya Kuaga (10 Hijria ) au kuchagua mwakilishi kama alivyomchagua Abubakar r.a (9 Hijria)

Pia Makhalifah mbalimbali baada ya kuondoka Mtume SAAW walishika na kuandama mwenendo huo kiasi kwamba katika kila Hijja hakukosekana Khalifah au mwakilishi wake. Jukumu la kuisimamia Hijja lilibebwa kwa umakini wa hali ya juu katika usimamizi na utendaji kwa kutengeneza mazingira mwanana na mepesi ya kuwawezesha mahujaji kuikamilisha ibada hii bila ya usumbufu kama uliopo leo.

Khilafah Uthmania chini ya Sultan Selim I mwaka wa 1517 ndio waliasisi jina la (Khadim al-Haramayn al-Sharifayn). Walilibeba jukumu hilo la uwajibu wa juu wa kisiasa na kidini kwa kulinda maeneo matakatifu ya Uislamu na kusimamia Hijja. https://hisartravel.com.au/the-ottoman-empire-and-hajj-guardians-of-the-pilgrimage-routes/

Wakati wa Sultan Bayezid I, Khilafah ilituma msafara kila msimu wa Hijja unaojulikana kama 'Surre' kutoka Istanbul hadi Makka ukibeba pesa, zawadi, na vifaa kwa ajili ya mahujaji.

Aidha, Khilafah Uthmania waliufanya mji wa Damascus kuwa kitovu kikuu cha kusimamia Hijja ili kusafirisha mahujaji kwa usalama kutoka kwa jiji. Pia wakachimba visima, wakaweka maghala, nyumba za wageni ili kuhakikisha uwepesi kwa mahujaji.

Na katika zama za Khalifah wa mwisho Abdul-HamidII, licha ya dola udorora kwa kubanwa na uadui wa makafiri na vibaraka ilitoa huduma kwa mahujaji kwa ikhlasi, kiasi cha kujenga 'Reli ya Hijaz' kuanzia mwaka 1900 na kufunguliwa rasmi Septemba 1908. Reli hii iliunganisha Makao makuu ya Khilafah Istanbul Uturuki na kupitia katika majimbo mbalimbali ya dola ikiwemo miji mikubwa ya Kiislamu ya Damascus Syria hadi ndani ya Madina katika nchi ya Hijaz. http://www.caliphate.eu/2008/04/hejaz-railroad-symbol-of-muslim-unity.html

Hijja yetu leo inapitia katika hali ngumu kigharama, kiusimamizi na kiutendaji kwa kuwa watawala wa Saudia hawana haja ya Uislamu. Ni wajibu kwa Umma wetu ufanye kazi ya kurejesha tena dola ya Khilafah itakayoanzia katika ulimwengu wa Kiislamu, ili ije isimamie ipasavyo ibada hii kwa kuondosha kila tabu, uzito na pingamizi zilizowekwa leo.

**Mhariri**

**01 Dhul Qa'ada 1446 Hijria**

**Mei 2025 M**

***jukwalakhilafah@gmail.com***

makwao. Mwaka 2008 matukio ya uvamizi dhidi ya wageni yalijiri tena hapo hapo (Johannesburg) kiasi cha kuwafukuza na kuwatoa kwenye makaazi yao maelfu ya wahamiaji, kulitendeka wizi mkubwa wa mali, biashara na wa majumbani, na idadi ya waliofariki kufikia hadi 56.

Pia mwaka 2015 matukio kama hayo yalitokea kufuatia kauli za uhamasishaji za Mfalme wa Wazulu Goodwill Zwelithini kaBhekuzulu alipowataka wahamiaji "wafunge virago vyao na kuondoka mara moja". Ndani ya mwezi Aprili mwaka huo huo (2015) watu saba waliuwawa, na wageni wengine zaidi ya 2000 walitolewa kwenye makaazi yao.

Bila ya kusahau pia Septemba 2019 kuliibuka machafuko ya kikatili na kuuwawa watu wasiopungua 12 wengi kutoka Nigeria. Hali hiyo ikapelekea ulipizaji kisasi nje ya Afrika ya Kusini. Nigeria ilimwita nyumbani balozi wake, kuanza zoezi la kuhamisha raia wake na kususia Mkutano wa Jukwaa la Uchumi la Kilimwengu kuhusu Afrika uliopangwa kufanyika mjini Capetown nchini humo.

Hali hii ya chuki dhidi ya wageni wanaoingia Afrika ya Kusini ni kutokana na dhana ya wananchi wa nchi hiyo kwamba wahamiaji wanapora fursa zao na ndio dhamana wa umaskini wao, badala ya wao kukabiliana na chanzo halisi, ambacho ni sera thakili za uchumi wa kibepari.

Mfumo wa kibepari waliorithi waafrika ya kusini kutoka kwa wakoloni wa Kiengereza umechochea hisia za kibaguzi za kiaswabia/utaifa hususan miongoni mwa vijana. Fikra za uchoyo wa kitaifa zimezuwa mauaji ya wengi, uporaji kwa jina la kuhami rasilmali za nchi kutokana na kuvamiwa na wageni.

Nidhamu ya uchumi ya kibepari imeisukumiza Afrika ya Kusini katika shimo kubwa la kukosekana uwiano wa kiuchumi baina ya wenye nacho na wasiokuwa nacho. (maskini na matajiri). Afrika ya Kusini imekua ni moja katika nchi ambayo imekosa kwa kiasi kikubwa uwiano na usawa huo wa kiuchumi baina ya raia wake. Wakati raia wao wengi wakimwaga lawama kwa wageni na kujijaza fikra za chuki dhidi ya wahamiaji, ukweli ni kuwa nchi hiyo inakabiliwa na changamoto nyingi na kubwa zaidi kuliko uwepo wa wageni.

Kwa mfano, madai kuwa wageni wamekua shehena katika huduma zao za kijamii ikiwemo suala la mpango wa Afya wa kitaifa, taarifa za serikali zinaonesha kwamba nchini humo kuna wageni 2.1 katika idadi yao ya watu 51.7 milioni. Idadi hiyo ni kwa mujibu wa hesabu ya 2011 (kwa sasa inawezekana idadi hiyo imeshapaa mpaka milioni 55.7).

Afrika ya Kusini licha ya kuitwa kuwa miongoni mwa vinara bora wa demokrasia, nchi ya pili kuwa na uchumi wa juu barani Afrika, ikiwa na miundo mbinu bora, nidhamu mwanana iliyoboreshwa ya masuala ya kifedha na kuwepo uzalishaji wa hali ya juu wa maadini na viwandani, ukweli uliopo bado nchi hiyo inakabiliwa na msinyao mkubwa katika uchumi wake husussan robo ya mwanzo ya mwaka 2019, pia ikikabiliwa msambaratiko mkubwa wa kijamii.

Kuhusiana na ukosefu wa ajira, suala hilo limekita na kutapakaa nchini Afrika ya Kusini, kiasi cha Raisi Ramaphosa kuwahi kusema kuwa ni "mgogoro mkubwa na wa hatari". Kwa mujibu wa data zilizotolewa mwezi Februari 2026 kiwango cha ukosefu wa ajira kitaifa ni 31.4%.

Sura pana katika jamii ya Afrika ya Kusini, ni kama zilivyo jamii nyengine chini ya ubepari, imeemewa na kuchanganyikiwa bila ya kuwa na suluhisho halisi kutatua matatizo yao ya kijamii, kisiasa na kiuchumi, na badala yake hukimbilia kulaumu na kuwasingizia wageni na wahamiaji wakiwa wao ndio mbuzi wa kafara, huku wanasiasa wakionekana kuyaunga mkono matukio ya chuki hizo kijanja, ikiwa ni mbinu yao ya wao kujikusuru (kukwepa lawama).

Uhalisia ni kuwa serikali imeshindwa kutatua matatizo yao yaliyoibuka kutokana na mfumo wa kibepari, na hivyo kuhamishia tatizo la umasikini kuwa linasababishwa na wageni na wahamiaji, kitu ambacho hatima yake huzua umwagaji damu na vurugu la ukatili kama zama za ubaguzi wa rangi au zaidi kamwe.

Zaidi ya hayo, vurugu hizi za chuki dhidi ya wageni Afrika ya Kusini zinafedhehi waziwazi fikra butu ya umoja wa waaafrika au 'Umajmui wa Afrika', yaani Afrika kwa waafrika. Kauli mbiu tupu bila ya uhalisia, kama

**Inaendelea uk 5**

## NUSRA INATAFUTWA KUTOKA KWA NANI?!

**Swali:**

Je, kuwasilisha Uislamu kama mradi wa hadhara kunahusiana tu na maeneo yenye nguvu ndani ya nchi za Kiislamu pekee? Au pia kunahusisha nchi zisizo za Kiislamu, kama alivyofanya Mtume Muhammad (?(ﷺ

**Jibu:**

Kutafuta Nusra (kuomba msaada) kunapaswa kufanywa kwa yule anayekubali Uislamu na kuuingia, na ambaye ni miongoni mwa watu wa nguvu na ulinzi, ili aweze kuinusuru dini na kusimamisha utawala kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu. Masharti haya mawili lazima yatimie kwa mnayeitafuta Nusra kwake. Ikiwa hatakubali Uislamu na kuuingia, au si katika watu wa nguvu na ulinzi wenye uwezo wa kuleta mabadiliko, peke yake au pamoja na wengine, basi hatakuwa miongoni mwa watu wa Nusra. Ama Quraysh, haikuwa hivyo kabla ya ufunguzi wa Makka; kwani watu wake wenye nguvu na ulinzi hawakuingia Uislamu wakati huo, hivyo Mtume ( (ﷺhakutafuta nusra yao. Bali alikuwa akilingania katika Uislamu huko Makka, na waliokubali walikuwa ni wanyonge na baadhi ya watu wenye nguvu kama watu binafsi bila makabila yao, hivyo hawakuwa na uwezo wa kuleta mabadiliko, kama Umar na Hamza (radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao). Kwa hiyo, hapakuwa na kutafuta Nusra kutoka kwa watu wa Makka kwa sababu masharti hayo mawili hayakutimia. Bali kulikuwa na da'wah ya Uislamu Makka, na hakuna waliokubali kutoka kwa watu wa




nguvu na ulinzi wenye uwezo wa kuleta mabadiliko; hivyo hapakuwa na *Talab an-Nusra* Makka, bali Makka ilifunguliwa kwa ushindi.

Ndiyo maana Mtume wa Mwenyezi Mungu ( (ﷺalikuwa akijiwasilisha kwa watu wa nguvu na ulinzi kutoka makabila; alikuwa akiwaalika kwanza katika Uislamu, na wakikubali ndipo anatafuta nusra yao. Miongoni mwa yaliyotajwa katika Sira:

**Kwanza: Kutoka Sira ya Ibn Hisham:**

**1- Kutafuta Nusra kutoka kwa Thaqif:**

... Mtume ( (ﷺalipofika Taif aliwaendea wakuu wa Thaqif, akakaa nao na kuwalingania kwa Mwenyezi Mungu na kuwaomba wamnusuru katika kueneza Uislamu... lakini walimjibu vibaya na hawakukubali, hivyo akaondoka kwao bila matumaini.

**2- Kutafuta Nusra kutoka kwa Bani Amir ibn Sa'sa'ah:**

... aliwalingania kwa Mwenyezi Mungu na kuwaomba nusra. Mmoja wao akasema: "Ikiwa tutakupa bay'ah kisha Mwenyezi Mungu akakupa ushindi, je, tutakuwa na mamlaka baada yako?"

Mtume ( (ﷺakasema: «الْأَمْرُ إِلَى اللهِ يَضَعُهُ حَيْثُ يَشَاءُ» **"Mamlaka ni ya Mwenyezi Mungu, huiweka anapotaka."** Wakasema: "Je, tujitoe kupigana na Waarabu kisha ukishinda mamlaka iwe kwa wengine? Hatuna haja na jambo lako." Hivyo wakamkataa.

**Pili: Kutoka kwa Tafsiri ya Ibn Kathir:**

["Kisha tukafika kwenye mkusanyiko uliojaa heshima ambapo kulikuwa na wazee kadhaa wa hadhi ya juu na mashuhuri. Abu Bakr aliwakaribia na kuwasalimia. Ali alisema: Abu Bakr alikuwa mtu wa kuchukua hatua katika kila tendo jema. Abu Bakr akawaambia: Nyinyi watu mnatoka wapi? Wakasema: Kutoka kabila la Banu Shayban bin Tha'laba. Kisha Abu Bakr akamgeukia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) na kusema: "Baba yangu na mama yangu na watolewe kafara kwa ajili yako! Hakuna mtu mwenye heshima zaidi katika kabila lao kuliko hawa!"

Mafrooq akasema: Unalingania nini, ewe kaka Mquraysh? Kisha Rasulullah (saw) akasongea mbele na kukaa, Abu Bakr akasimama na kumfunika Rasulullah (saw) kwa nguo zake. Rasulullah (saw) akasema:

**"Ninakulinganieni ushuhudia kwamba hakuna anayestahili kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu Mmoja na kushuhudia kwamba mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Pia naomba munipe ulinzi na nusra ili niweze kufikisha ujumbe ambao**

**Inaendelea uk .5**

**Mwenyezi Mungu ameniamuru niupitishe, kwa sababu Maqураysh wameungana dhidi ya Dini ya Mwenyezi Mungu; wamemkataa Mtume Wake, na wameridhika na batili badala ya haki. Lakini Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujitegemea, Anayestahiki Sifa zote."**

Muthanna akasema, "Ndugu Mqurayshi! Nimesikiliza ulichosema. Ninapenda ulichosema kwani kimenivutia sana. Hata hivyo, jibu langu kwako litakuwa jibu lile lile ambalo Haani bin Qabeesah ametoa; tunajikuta katikati ya mipaka ya nchi mbili. Moja ni Yamaamah na nyingine ni Samaawah."

Rasulullaah (saw) alimuuliza, «وما هذان الصريان؟» **"Mko kwenye mipaka ya nchi zipi mbili?"** Akajibu, "Upande mmoja nasi tuna ardhi, vilima virefu na milima ya Waarabu huku upande mwingine tuna ardhi ya Wafursi na mito ya Kisra. Kisra imeturuhusu kuishi huko kwa sharti kwamba tusianzishe chochote kipya na tusimuunge mkono mtu yeyote anayeanzisha harakati mpya. Uwezekano ni mkubwa kwamba wafalme wa Fursi hawatapenda kile unachotuitia, ilhali desturi katika nchi ya Waarabu ni kuwasamehe wale watakaokuwa wamekosea na kukubali udhuru wao; desturi ya nchi ya Wafursi ni kwamba watu wanaofanya makosa hawasamehewi wala udhuru wao haukubaliwi. Kwa hivyo, ikiwa mnataka tuwarudishe kwenye nchi yetu na kuwanusuru dhidi ya Waarabu, tunaweza kukubali jukumu hili" Rasulullaah (saw) aliwaambia,

**«ما أسأتم الرد إذ أفصحتم بالصدق، إنه لا يقوم بدين الله إلا من حاطه من جميع جوانبه» "Jibu lenu halijawa baya kwa sababu mumesema ukweli. Hata hivyo, watu pekee wanaoweza kusimamisha Dini ya Mwenyezi Mungu ni wale wanaoilinda kutoka kila pembe." 24/6/2021] Mwisho wa Nukuu.**

**Tatu:** kama inavyoonekana, Mtume (ﷺ) alikuwa akiwaalika kwanza katika Uislamu kisha anaomba nusra yao. Wakikubali kwa uaminifu na wakawa na nguvu na uwezo wa kusimamisha utawala wa Kiislamu, ndipo anaomba nusra yao. Ama wakitoa masharti ya kidunia, kama kutaka wao watawale baada yake au kuchagua kupigana na baadhi ya watu tu, basi hilo halikubaliwi. Ndiyo maana katika Bay'at al-Aqaba, Ansar walipouliza: "Tutapata nini tukikuhami?" Mtume (ﷺ) akasema: "Pepo." Hawakuweka masharti ya kidunia.

**Katika Sira ya Ibn Hisham (1/446) - Sura kuhusu maneno ya al-Abbas ibn Ubadah kwa Khazraj kabla ya kiapo cha utiifu:**

**...]** [Ibn Ishaq alisema: Asim ibn Umar ibn Qatada aliniambia: Watu walipokusanyika kutoa kiapo cha utiifu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), al-Abbas ibn Ubadah ibn Nadhlah al-Ansari, ndugu wa Banu Salim ibn Awf, alisema: "Enyi watu wa Khazraj, mnajua mnachotoa kiapo cha utiifu kwa mtu huyu?" Wakasema: "Ndiyo." Akasema: "Mnatoa kiapo cha utiifu

**Inaendelea uk 8**



ilivyo fikra ya 'Umajmui wa Waarabu'.

Aidha, ni kielelezo cha fedheha ya wazi ya kushindwa dhana ya ukabila, fungamano duni na tete mno, kwa kuwa baadhi ya jamii za makabila zinazoishi Afrika ya Kusini kama Wazulu na Xhosa ndio jamii za makabila ya watu hao hao yanaoishi katika nchi jirani kama Botswana, Lesotho, Zimbwabwe, Malawi, Msumbiji nk. lakini bado watu hao hawa salimiki katika kudhuriwa kwa ukatili na wimbi hili la chuki za ubaguzi dhidi ya wageni, wakihesabiwa kuwa nao ni wageni

Ni wazi ubepari umeshindwa katika sekta ya kiuchumi na kijamii, unazalisha umasikini na kutengeneza pengo baina ya wenye nacho na wanyonge kwa kiasi cha kutisha, unazalisha husuma / uadui ukikosa fungamano thabiti na imara kuwafungamanisha watu pamoja. Tumaini pekee la kuuokoa ulimwengu kutokana na minyonyoro ya ubepari ni Uislamu chini ya dola yake ya Khilafah Rashidah.

*********************



# MKATABA WA HILF AL-FUDHOUL UTUONGEZE HIMA YA ULINGANIZI

Katika mwezi kama huu wa Qhulqaadah katika zama za Jahilia, kabla Mtume SAAW hajapewa Utume baadhi ya makabila makubwa ndani ya Makka walifanya mkataba unaoitwa Hilf al-Fudhoul wenye lengo la kuzuiya dhulma na kuwatetea wanyonge, wageni na wanaodhulumiwa.

Mkataba huo ulifanyika wakati Mtume SAAW akiwa bado kijana sana akijumuika na ami yake kwa kushiriki kikamilifu katika kikao kilichopelekea makubaliano ya mkataba huo.


Na mara baaada ya Mtume SAAW kupewa Utume aliyataja, kuyasifu na kuunga mkono kwa dhati makubaliano hayo.

Mazingira yaliyopelekea makubaliano ya mkataba huo yalikuwa kama hivi:

Mfanyabiashara mmoja wa Yemen kutoka kabila la Zabid alileta bidhaa na biashara zake ndani ya mji wa Makka akampatia bidhaa zile mmoja katika mabwanyenye wa Makka kwa jina la Ass bin Wail Al-Sahm (baba wa sahaba mkubwa Amr ibn-ul Ass). Bwanyenye huyu kwa kujiona ni katika watu wenye athari, ushawishi mkubwa ndani ya Makka na kuona kwamba mfanyabiashara huyu ni mnyonge na mgeni mjini pale hana wa kumtetea alikataa kumpatia malipo ya bidhaa alizochukua kutoka kwake.

Mfanyabiashara yule kutoka Yemen akajaribu kila hali kumshawishi bwana Ass bin Wail ampatie haki yake lakini akakataa kumpatia haki yake hiyo.

Mfanyabiashara huyo kutoka Yemen akajaribu kupita huku na




kule kutaka kuungwa mkono na Makureishi na kutoa kilio chake kwa watu wa Makka ili wamsaidie ili aweze kupata haki yake lakini ilishindikana.

Hata hivyo, mfanyabiashara huyo bado alifanya ujasiri hakukata tamaa katika kutafuta haki yake, aliendelea kufanya jitihada kwa kupanda juu ya mlima unaoitwa Abu Qubays karibu na Masjid Haraam, hapo akanadi tena na tena kwa mashairi akipaza sauti ya kilio na masikitiko yake juu ya dhulma aliyofanyiwa katika biashara yake.

Hatimaye ami wa Mtume SAAW bwana Al-Zubayr bin 'Abd al-Muttalib akaguswa na kilio na hali ya dhulma aliyotendewa mfanyabiashara yule, akaona kuna haja ya kuchukua hatua ya kumpigania haki yake na kuzuiya dhulma kama zile zisitokee.

Bwana Al-Zubayr bin 'Abd al-Muttalib akayakusanya baadhi ya makabila mashuhuri ndani ya Makka, kama vile: Banu Hashim, Banu l-Muttalib, Banu 'Abd Manaf, Banu Zuhra bin Kilab, Banu Taym bin Murra, Banu Asad bin Abd al-'Uzza bin Qusay na kuitisha kikao maalum katika nyumba ya bwana Abd Allah bin Jud'an al-Taymi kuzungumzia namna ya kumsaidia mfanyabiashara yule, lakini pia kuja na maazimio ya kutowadhulumu watu haki zao Maazimio muhimu ya kikao kile yalikuwa:

a. Mtu yoyote husuan mgeni asidhulumiwe haki yake kwa namna yoyote.

b. Lau kuna mtu kadhulumiwa na kuna mtu hataki kumpa haki aliyemdhulumu, makabila ya mktaba huo yasimame dhidi ya dhalimu, kwa ajili ya kumtetea aliyedhulumiwa.

Mkutano ule ndio uliozaa mkataba wa makubaliano adhimu (Hilf alfudhoul) ambayo Mtume SAAW baada ya kupewa Utume aliyasifu na kuyaunga mkono kwa kusema:

"Nilishuhudia makubaliano katika nyumba ya Abdallah bin Jud'an ambayo kamwe nisengependa kuyavunja hata kama nikipewa ngamia wote wekundu. Lau leo ningeitwa tena (kwa makubaliano kama yale) basi ningekubaliana nayo."

Mafundisho matatu makubwa yanapatikana katika tukio na mchakato wa kupatikana mkataba huu:

Kwanza, lau mfanyabiashara wa Yemen aliyeleta bidhaa zake Makka na kudhulumiwa angekata tamaa na kwa kujiona mnyonge, dhaifu na mgeni pale Makka bila ya kupaza sauti yake kupigania haki yake na kupambana na dhulma basi angemalizia kwa kukosa haki yake daima.

Pili, wakati wote katika maisha ya wanadamu kuna watu ambao huguswa na kuchukizwa na Uk. 8

kiuchumi na kisiasa za ubepari mamboleo, ikiwemo ubinafsishaji, kuondoa udhibiti wa serikali (deregulation),biashara huria, pamoja na kupunguza kwa kiwango kikubwa matumizi ya umma, nk.

Kwa upande wa kisiasa, Tanzania ilichukuwa mfumo wa vyama vingi mwaka 1992 baada ya miaka thelathini ya utawala wa chama kimoja, na hivyo kuhalalisha vyama vya upinzani, pamoja na ukweli kuwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimeendelea kubaki chama tawala chenye nguvu katika kila uchaguzi mkuu tangu wakati huo.

Ingawa rasmi Tanzania inashikilia demokrasia ya vyama vingi, huku uchaguzi wake wa kwanza ukiwa mwaka 1995, mazingira ya kisiasa yamekuwa yakikumbwa na vurugu za mara kwa mara katika kila uchaguzi. Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 wa muhula wa pili wa Rais Samia, zoezi hilo liligubikwa na vurugu kali kwa siku kadhaa kuanzia tarehe 29 Oktoba 2025, zilizosababisha hasara kubwa ya maisha ya watu, mali, na miundombinu ya umma.

Pia, miongoni mwa vurugu mbaya zaidi zilizohusiana na uchaguzi ni zile za mwaka 2000 huko Zanzibar, ambapo watu 35 waliuawa, 600 walijeruhiwa na takribani watu 2,000 walikimbilia Kenya.

Kwa kuwa Tanzania imekua chini ya ushawishi wa Uingereza tangu enzi za ukoloni hadi kupata uhuru wake mwaka 1961, Uingereza kama dola bwana yenye ushawishi mkubwa imekuwa ikichukua hatua za haraka kuingilia kati kila panapotokea hali ya sintofahamu ya kisiasa kupitia jukwaa la Jumuiya ya Madola, kwa lengo la kurejesha utulivu na kulinda ushawishi na nguvu zake, pamoja na kuzuiya kupenya kwa ushawishi wa Marekani. Kwa mfano, mwaka 1996, pale mvutano wa kisiasa na mkwamo ulipotokea Zanzibar kati ya CCM na CUF, Jumuiya ya Madola ilimtuma Katibu Mkuu wake, Chief Emeka Anyaoku, kama mpatanishi mkuu wa kidiplomasia ili kuratibu makubaliano ya kugawana madaraka kati ya vyama hivyo viwili vilivyokuwa vikikinzana.

Kwa uhalisia, wajumbe wa Jumuiya ya Madola kimsingi hawaji kutatua mivutano ya kisiasa, kwani demokrasia yenyewe kimaumbile inaambatana na vurugu na mvutano. Mfano hai wa hili ni Zanzibar ambako bado kuna kuyumbayumba kwa utulivu wa kisiasa. Hata hivyo, lengo kuu la Jumuiya ya Madola ni kuhifadhi na kudumisha ushawishi wa Uingereza katika eneo husika.

Zaidi ya hayo, ujio wa wajumbe hawa (wa Jumuiya ya Madola) unaonyesha hali ya kusikitisha kwa namna gani nchi zinazoendelea barani Afrika na kwingineko bado haziko huru kikamilifu, hazijitoshelezi, wala hazina uwezo wa kutatua hata matatizo yao wenyewe. Aidha, hata mashirika yao ya kikanda kama Jumuiya ya Afrika Mashariki, wala yale ya bara zima kama Umoja wa Afrika (AU), hushindwa kuikoa hali, kuamua au kutatua chochote katika qadhia za nchi zao, badala yake hulazimika kupokea maelekezo na masuluhisho ya uwongo kutoka kwa mataifa ya kikoloni kutoka London, Washington, Paris, na kwengineko.

Wakoloni, nchi za kibepari za Magharibi, daima wanachochea machafuko, vurugu na umwagaji damu barani Afrika kwa kutumia pande pinzani na kugawa silaha kwa makundi haya pinzani kwa ajili ya maslahi yao binafsi, kisiasa na kiuchumi. Mara pale damu inapomwagika, hujifanya kuleta wajumbe, kuunda tume na kutuma ujumbe— si kwa ajili ya kuchunguza kwa dhati kilichotokea, bali kama nyenzo za kuzinyenyekeza serikali za nchi zinazoendelea.

Afrika haijawahi kuwa katika amani na utulivu tangu uvamizi wa wakoloni wa magharibi, na hata baada ya kupata uhuru wa bendera katika miaka ya 1960. Ni wakati muafaka kwa watu wa Afrika kuukumbatia na kuunga mkono Uislamu, kwani kupitia dola yake ya Khilafah utaleta amani, haki, kukomesha umwagaji damu na unyonyaji dhidi ya Waislamu na wanadamu kwa ujumla, pamoja na kuwafukuza wakoloni wote— kama ilivyotokea wakati Wareno walipovamia Afrika Mashariki katika karne ya 17 BK.

**Imeandikwa na Said Bitomwa**
**Mjumbe wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania**
**Kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

*****************



## Nusra.. kutoka uk 4

Nusra.. kutoka uk 4

kwake ili kupigana na watu wote, bila kujali rangi. Mkifikiri kwamba ikiwa mali zenu zitapungua na viongozi wenu watauawa, mtamsalimisha, basi fanyeni hivyo sasa. Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, mkifanya hivyo, itakuwa fedheha katika dunia hii na Akhera. Lakini mkifikiri kwamba mtakuwa waaminifu kwa kile mlichomwita, hata kwa gharama ya mali zenu na kupoteza viongozi wenu, basi mchukueni. Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, itakuwa jambo bora zaidi katika dunia hii na Akhera." Wakasema: "Tutamchukua hata kwa gharama ya mali zetu na hasara ya viongozi wetu. **Tutapata faida gani kutokana na hilo, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ikiwa sisi ni waaminifu?" Akasema: "Pepo." Wakasema: "Nyoosha mkono wako." Akanyoosha mkono wake nao wakaapa utiifu kwake].**

**Kwa kumalizia: Nusra hutafutwa kutoka kwa wale wanaokubali Uislamu na kuuingia, na ambao ni watu wa nguvu na ulinzi wenye uwezo wa kuinusuru dini na kusimamisha hukmu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, peke yao au pamoja na wengine. Ikiwa hawatakubali Uislamu au hawana nguvu na uwezo wa kuleta mabadiliko, basi hawahesabiwi kuwa ni miongoni mwa watu wa Nusra.**

**Natarajia haya yanatosha, na Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi na Mwenye hekima. ]] Mwisho wa nukuu.**

**Ndugu yenu,**

**Ata bin Khalil Abu Al-Rashtah**

9 Shawwal 1447 H -

27/3/2026 M

## Hilf al-fudhoul … **Kutoka uk. 6**

huguswa na kuchukizwa na dhulma kwa misingi ya ubinadamu, na huwa wako tayari kwa hali zote kusimama kidete kuwasaidia wanaodhulumiwa dhidi ya madhalimu.

Tatu, ni namna Uislamu usivyopenda dhulma, na ndio maana Mtume SAAW akasema hata angeitwa tena katika mkataba ule wa kupambana na udhalimu basi angeunga mkono makubaliano yale. Hilo ni fundisho la kudumu kwetu kusimama imara kuwatetea waliodhulumiwa na kuwapinga madhalimu.

Tukio hili lizidishe hima na ghera yetu kusimama kukataa dhulma kwa sura zake zote, ikiwemo kutetea ndugu zetu walioko mahabusu kwa kesi za uonevu za kubambikiwa za ugaidi. Lakini kubwa zaidi ni kufanya ulinganizi wa kurejesha tena dola ya Kiislamu (Khilafah) itakayoanzia katika biladi kubwa za Waislamu, kwa kuwa dola hiyo ndiyo pekee yenye uwezo wa kuzuiya na kupambana na dhulma dhidi ya Waislamu na wanadamu kwa jumla.

****TUNAWATAKIA KILA LA KHERI MAHUJAJI WOTE ULIMWENGU MZIMA**

*****************

## MATUKIO YA MWEZI MEI

1/05 Siku ya Wafanyakazi duniani.

1/05 1707 - Siku ya Muungano baina ya England na Scotland kuunda dola ya Great Britain. Wales ilikuwa tayari ndani ya Muungano huo tangu miaka 1500's.

2/05 2011 – Kikosi malumu cha Marekani kilimuuwa kwa dhulma Sheikh Usamah bin Laden (Allah Amrehemu) nyumbani kwake mjini Abbotabad, Pakistan.

3/05 – Siku ya Uhuru kwa Vyombo vya Habari

5/05 Mwanafikra mkubwa wa mfumo wa kikafiri wa kikomunisti myahudi Karl Marx (1818-1883) alizaliwa mjini Treves, Germany.. Miongoni mwa maandishi yake ni vitabu cha *Das Kapital* na *The Communist Manifesto,*

7/05 1915 -. Meli ya Uiengereza inayoitwa *Lusitania* ilipigwa mabomu na nyambizi (sub marine) ya kivita ya Ujerumani. Kwa kuwa miongoni mwa abiria wengi pia walikuwa wamarekani. Mashambulizi haya yalichangia kuishawishi Marekani kujitosa katika Vita vya Kwanza vya Dunia.

8/05/ 1945 Kumalizika Vita Vya Pili Vya Dunia ndani ya Ulaya

8/05 Siku ya Red Cross duniani kufuatia kuzaliwa Henri Dunant (1828-1910) Mwasisi wa Jumuiya hiyo. Alizaliwa mjini Geneva. Yeye pia ndie mwasisi wa taasisi inayoitwa YMCA

9/05 Siku ya Mama ndani ya Marekani na Canada

9/05 Jeshi la Italia laivamia Ethiopia